**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA ARDHI NA MAWASILIANO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,**
Hatuna budi kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima tukaweza kukutana tena katika Mkutano wa Sita kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili kuweza kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,**
Nichukuwe nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, Mheshimiwa Salama Aboud Talib, Naibu Waziri, Mheshimiwa Juma Makungu Juma, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukifanya kazi zetu za kawaida za Kamati. Tunawashukuru sana.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, napenda kuipongeza tena Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa umahiri na ufanisi wa hali ya juu kabisa katika mfumo huu wa bajeti unaozingatia programu ya "PBB" (Program Based Budget).

**Mheshimiwa Spika,**

Sambamba na hilo, sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za pekee kwa Wajumbe wa Kamati yangu na Katibu, ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuyapitia na kuyachambua makadirio haya ya Bajeti ya Wizara hii na hatimaye kuyakubali bila ya marekebisho yoyote.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kuheshimu, kuthamini na kutambuwa mchango wao mkubwa kwenye Kamati hii hadi kufanikisha kazi hii iliyokusudiwa, naomba niwataje kwa majina Wajumbe na Katibu wa Kamati hii ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Suleiman Sarhan Said - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Khadija Omar Kibano - Mjumbe
4. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe
5. Mhe. Mohamedraza Hassanali - Mjumbe
6. Mhe. Nassor Salim Ali - Mjumbe
7. Mhe. Said Omar Said - Mjumbe
8. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Baraza la Wawakilishi liliidhinishia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Matumizi yenye jumla ya Tshs. 9.555 bilioni kwa ajili ya Fungu N01 kwa Matumizi ya kazi za Kawaida. Aidha, Baraza pia liliidhinishia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kutumia jumla ya Tshs. 47.900 bilioni kwa ajili ya Matumizi ya kazi za Maendeleo. Vile vile, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumlaya Tshs. 6.100 bilioni kama ni mapato yatokanayo na vyanzo mbali mbali vinavyosimamiwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 Wizara hii imepangiwa Tshs. 10.664 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tshs. 36.943 bilioni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, inakadiriwa kutumiaTshs. 47.608 bilioni kwa ajili ya utekelezaji mzima wa Fungu N01. Aidha, katika utaratibu mpya wa bajeti

inayozingatia programu ya 'PBB', Wizara hii imepangiwa kutekeleza Programu Kuu Nne (4) na Programu Ndogo Nane (8) kama zilivyofafanuliwa katika hotuba hiyo ya bajeti ya Wizara hii ya Ardhi, Maji Nishati na Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya maelezo hayo sasa naomba kwa idhini yako Mhesimiwa Spika nianze na uchambuzi wa Programu hizo kama zilivyokwishatangulia kuelezwa na Mhe. Waziri katika kitabu chake cha hotuba aliyoiwasilisha mbele yetu muda mchache uliopita.

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,**
Kama inavyofahamika kuwa jukumu kubwa la Programu hii ni kuimarisha shughuli za uratibu katika suala zima la utekelezaji wa kazi za Wizara pamoja na kukuza ufanisi katika utawala wa rasilimali ardhi pamoja na utoaji wa huduma kwa jamii. Aidha, Programu hii inajumuisha Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Afisi Kuu Pemba ambapo jumla yaTshs. 2,040,551,000 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii. Vilevile, programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo zake tatu (3).

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**
Kupitia Programu Ndogo hii, Kamati yangu inamuomba Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Tume ya Kurekebisha Sheria kuweza kuharakikisha ufanyaji wa marekebisho ya baadhi ya Sheria mbali mbali zinazohusiana na maswali mtambuka ya ardhi katika Visiwa vyetu na ambazo husababisha mtafaruku mkubwa na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi ambapo hadi kufika mwezi Machi, 2017, jumla ya kesi 473 zimepokelewa ambapo ni kesi 241 tu ambazo zimetolewa maamuzi kwa upande wa Unguja na Pemba. Maoni ya Kamati yangu katika eneo hili ni kumtaka Waziri kusimamia watendaji wake vizuri ili kuweza kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kuzipitia Sheria zote za ardhi ili kupata Sheria bora inayoendana na wakati huu na hivyo kuleta maslahi mapana kwa wananchi wetu pamoja na wawekezaji kutoka nje ya nchi. Aidha, kwa vile Tume ya Kurekebisha Sheria tayari wameshazipitia karibu Sheria zote na kuona wapi

kwenye utata, kazi iliyobaki ni kukaa na Wizara ili kuzifanyia kazi na kupata Sheria bora.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hiyo ya kusuasua kwa upande wa utoaji wa ardhi na kupelekea kuongezeka kwa migogoro hiyo sugu, Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kwa Bajeti hii tunayoipitisha ya 2017/2018 kuhakikisha wanaandaa sera mpya ya ardhi na hatimaye kuweza kuzifanyia marekebisho baadhi ya Sheria hizo nakuja na Sheria mpya mbele ya Baraza lako hili katika kikao kinachofuata kama tulivyoshauri hapo juu.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UPANGAJI WA MATUMIZI YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa majukumu makuu ya Programu kuu hii ni kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi kwa maendeleo ya nchi pamoja na kuwa na matumizi yaliyo bora na yaliyo na fanisi. Aidha, Programu hii kawaida hutekelezwa na taasisi mbali mbali kama Idara ya Ardhi, Afisi ya Usajili wa Ardhi, Idara ya Upimaji na Ramani na Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Hata hivyo, Mahakama ya Ardhi nayo inahusika na utekelezaji wa programu hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Hivi sasa kumekuwa na miradi mingi mikubwa ya uwekezaji hasa katika Mji wa Fumba, Mbweni n.k. Kamati yangu haijaridhika na mfumo wa ujenzi unaoendelea katika maeneo hayo kwa ajili ya kujenga nyumba za kisasa bila ya kuzingatia ukubwa wa ardhi yetu ya Zanzibar tulionayo kuwa ni ndogo. Aidha, uwekezaji huo umeanza kwa ujenzi wa majengo madogo ya ghorofa moja na mbili wakati ukiangalia eneo kubwa limeshapotea kwa maslahi ya wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiomba Serikali kutoruhusu tena ujenzi kama huo kwani watu wengi tulitengemea ujenzi huo utaanza na ghorofa saba na kuendelea ili kuweza kulinda eneo ndogo la ardhi tulilonalo na kuweza kubadilisha mandhari na haiba ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

## PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA WA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nieleze wazi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kuwa moja kati ya Programu muhimu katika Wizara hii ni programu ndogo hii ya Utawala wa Ardhi ambapo programu hii kwa mfumo wa hivi sasa moja kwa moja husimamiwa na Kamisheni ya Ardhi kwa kushirikiana na baadhi ya Idara kama nilivyozielezea hapo juu. Hata hivyo, Kamati yangu hairidhishwi na utendaji kazi wa Kamisheni hii ya Ardhi hususan katika masuala mazima yanayohusiana na uombaji wa ardhi, utoaji wa ardhi, upimaji pamoja na usimamiaji wa ardhi kwani changamoto sungu ni suala mtambuka kwani kila mmoja wetu anafahamu kuwa kila siku zikiendelea migogoro ya ardhi hapa nchini mwetu inazidi kuchuka nafasi na imekuwa ni kitu kisichoepukika.

**Mheshimiwa Spika,**

Hapa nitatoa mifano michache kati ya mingi ambayo imekuwa ni donda ndugu lisilopoa ambapo Baraza lako tukufu linatakiwa kufanya maamuzi magumu ili wananchi waweze kupata haki zao hasa katika maeneo yao yaliyochukuliwa kwa nguvu na baadhi ya viongozi bila ya ridhaa yao. Naamini hotuba ya Kamati yangu hii nnayoisoma hivi sasa itachambua tu baadhi ya kadhia hizo ambazo tutazitaja lakini Wajumbe wenzetu na nyie mnayajua mengi zaidi ya haya tutakayoyataja kwenye kadhi hii ya migogoro ya ardhi ambazo zimechukuliwa kutoka kwa wananchi walio wanyonge na viongozi wao kwa maslahi yao binafsi ambapo Kamati inaamini Wajumbe nao watapokuja kuichangia hotuba ya Wizara hii watayataja zaidi ya hayo tulioyaorodhesha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na kadhia hiyo, Kamati yangu ilihitaji na kuomba maelezo ya kina wakati wa kupitia bajeti kwa upande wa Wizara hii ili kuweza kujua ni kitu gani kinachopelekea kukiukwa kwa taratibu zilizowekwa na Sheria husika. Mfano wa baadhi ya kadhia hizo ni kama ifuatavyo:-

1. Mradi wa uwekezaji wa "Spice Islander" uliopo katika eneo la Nungwi lenye kilomita 7.8 ambapo muwekezaji huyo alipewa 'lease' halali ya eneo hilo na Serikali na baadaye kufutwa 'lease' hiyo bila ya taarifa kinyume na utaratibu wa Sheria na hatimaye kugaiwa ardhi hiyo kwa watu wengine wanne binafsi kinyume na Sheria ambapo kitu cha kushangaza ni kwamba ardhi hiyo aliyonyang'anywa muwekezaji na

kupewa watu ambao hawana hata mradi wa kufanya, matokeo yake wakawa wanatafuta wawekezaji ili kuyauza na kujipatia pesa kinyume cha Sheria ambapo jambo hilo ni utapeli na pia utakatishaji wa fedha chafu (yaani 'Money loundry') jambo ambalo ni uvunjifu wa Sheria za nchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na kadhia hiyo, tunamshukuru Makamo wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi baada ya kugundua dhulma imefanyika akaagiza kwa maandishi kuwa eneo hilo arejeshewe Muwekezaji wa 'Spice Islander' lakini cha kushangaza watendaji wa Wizara hiyo wamekusudia kumrejeshea robo tatu tu ya eneo hilo na robo moja hawataki kumrejeshea eti kwa sababu amepewa mtu mkubwa. Sasa suala hili ndio Kamati yangu inajiuliza hawa watendaji wetu wanafuata maelekezo kutoka kwa nani wakati Makamo wa Pili wa Rais ndiye kiongozi wa shughuli zote za Serikali? Kamati yangu inamtaka Waziri wa Ardhi alitekeleze agizo la Makamo wa Pili Rais kwa vitendo ili kulinda heshima ya Serikali, na huyo 'mtu mkubwa' atafutiwe eneo jingine kama itaonekana iko haja ya kufanya hivyo.

**MheshimiwaSpika,**

2. Suala jengine ambapo Kamati yangu haikuridhika ni kitendo alichofanyiwa muwekezaji kutoka nje wa Kampuni ya 'Pakachi Beach Resort' ambapo alipewa 'invoice' na Idara hii ili afanye malipo ya kupatiwa 'lease' hiyo lakini kitu cha kushagaza 'lease' hiyo imetolewa kwa jina la ndugu Mohamed Othman Abdalla ambapo Kamati yangu inahisi huo ni utapeli aliofanyiwa muwekezaji huyo wa kigeni ambapo aliifuata Kamati na tuliwaita Mkuu wa Wilaya ya Kusini, Sheha, Diwani, Mwenyekiti wa Halmashauri, Mmiliki alieuza eneo hilo mbele ya Waziri pamoja na watendaji wa Kamisheni ya Ardhi na kikao kilithibitisha kuwa 'lease' hiyo imetolewa kimakosa na ifutwe na itolewe nyingine kwa alielipa 'Invoice' kwa Serikali. Kitu cha kushangaza hadi leo hii 'lease' hiyo haijafutwa na kutolewa nyingine ambapo kwa lugha nyepesi Serikali imemtapeli muwekezaji huyo. Katika kadhi hiyo maoni ya Kamati kwa Waziri ni kuifuta 'lease' iliyotolewa kimakosa na itolewe nyingine kama 'invoice' iliyolipwa na muwekezaji wa Kampuni ya **'Pakachi Beach Resort'** ili kulinda heshima ya Serikali yetu kwa wananchi na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika,

3. Kamati yangu pia haikuridhika na tabia ya Kamisheni hii ya kuwanyima kuwapatia 'lease' baadhi ya wawekezaji hasa wazalendo bila ya kuwa na sababu madhubuti na kupelekea kuwarejesha nyuma katika kushiriki kwao katika uwekezaji. Mfano hai ni uwekezaji mkubwa uliopo huko Mangapwani ambapo muwekezaji mzalendo ndugu Khamis Kipara anakusudia kuekeza kwenye ujenzi wa Chelezo cha kutengezea Meli. Jambo la kushangaza ni kuwa hadi leo hii Kamisheni hawajampatia 'lease' ambapo majirani zake karibu wote ambao wamemkuta wao tayari wameshapatiwa 'lease'. Huu ni ubaguzi usio na sababu. Hivyo Kamati yangu inamshauri Mhe. Waziri kumpatia 'lease' muwekezaji huyo mzalendo kwani Kamati yangu ilpotembelea Mombasa (Kenya) iliukuta mradi kama huu ambao umetoa ajira nyingi kwa vijana. Hivyo, mradi huu wa muwekezaji mzalendo unaotaka kuwekweza hapa Zanzibar, si tu utaongeza ajira kwa vijana lakini pia utaongeza mapato ya pesa za kigeni hapo utakapoanza kazi. Wapo wawekezaji ambao wanakuja na kutaka kuingia ubia na kuwa tayari kushirikiana nae katika kuendeleza mradi huo lakini anashindwa kwa sababu hajapata 'lease' hadi leo. Na suala hili hapa Barazani sio jipya kwani hata Kamati iliyopita iliwahi kulisemea sana suala hili. Sasa sababu hatuelewi wakati mpaka EIA imeshatolewa? Hapa Waziri aje atuambie sababu za msingi vinginevyo ampatie 'lease' muekezaji huyo ili aendeleze mradi wake huo, tena kwa kupokea hoja yetu hiyo kuwa mradi huo hauwezi kufanyika katika eneo jengine lolote kwa hapa Unguja isipokuwa katika eneo hilo kwani lina kina kirefu cha maji ambacho meli ya ukubwa wowote inaweza kukaa katika eneo hilo ambalo ni adimu kwa hapa Zanzibar bila ya athari yoyote.

Mheshimiwa Spika,

4. Kadhia nyingine ambayo Kamati yangu haijaridhika na vitendo vilivyofanywa na aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo ni kuwanyang'anya eneo lao watu wa Nungwi na kumpatia mwananchi mwengine wa familia ya kubwa bila ya ridhaa yao ambapo wananchi hao wameshalalamika katika ngazi zote Serikalini hadi kufika Baraza la Wawakilishi ili kuwasimamia katika kupata haki yao hiyo. Na hivi sasa suala hilo tumepata taarifa kuwa limeshafikishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Kamati yangu inamtaka Mhe. Waziri kufuatilia hati hiyo iliyotolewa kimakosa kwa mwananchi huyo wa familia ya wakubwa na kurejeshwa ardhi hiyo kwa wananchi wanyonge walioporwa.

**MheshimiwaSpika,**

Kutumia nguvu na kuwadhulumu wananchi haki yao ya matumizi ya ardhi nakupewa mtu fulani kwa manufaa yake binafsi wakati tunapopewa dhamana na wananchi ili kuwaongoza, ni jambo baya sana ambalo huipelekea wananchi kukosa imani na Serikali yao inayowaongoza kwa vitendo vya watu wachache kwa maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika,**

5. Hali kadhalika na kwa upande wa Pemba eneo la Wingwi (Micheweni) nako pia wananchi wamenyanganywa ardhi ambapo walikua wakilima kwa ushirika na kupewa mtu wa familia hiyo fulani ambapo ardhi hiyo tangu siku hiyo aliopewa ipo tu na wala haitumiki kwa shughuli yoyote. Huku ni kuwarejesha nyuma wananchi wetu pia ni jambo ambalo ni kinyume cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa mujibu wa kifungu cha … kuyatumia madaraka aliyopewa kujinufaisha yeye mwenyewe au familia. Kwa hiyo, Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika ni nyema ardhi hiyo kuwarejeshea wananchi hao ili kuweza kutumika kwa maslahi ya umma.

**Mheshimiwa Spika,**

6. Vile vile, eneo la Muyuni Matemwe kuna mwananchi wa kijiji hicho Ndugu Choroko nae pia Wizara ilimtaka eneo lake ampatie muwekezaji kwa kukubaliana na Wizara kuwa muwekezaji huyo atampatia mwananchi huyo Tshs. 120 milioni ili atoe eneo hilo. Ila jambo la kushangaza ni kuwa kabla ya kulipwa fidia hiyo kwa mwananchi huyo Waziri aliyekuwepo katika Wizara hii alitoa 'lease' hiyo kwa muwekezaji huyo Ndugu Yakub. Na cha kusikitisha zaidi ni kuwa hadi hii leo tunasoma hotuba hii mbele yenu, mmiliki wa eneo hilo Ndugu Choroko hakulipwa hata senti moja lakini aliitwa Wizarani na watendaji wa Wizara hii na kupewa Tshs. 12 milioni na jibu alilopewa kuwa muwekezaji yumo anamtafutia pesa zake na zikishapatikana atakuja kumaliziwa. Suala la kujiuliza hapa ni kwa nini aliitwa Wizara na kulipwa pesa na mtendaji wa Serikali kwa niaba ya muwekezaji. Hali hiyo inaonyesha wazi kuwa watendaji wa Wizara kwa wakati huo walikuwa wanafanya pia kazi za udalali wa maeneo ya watu wanyonge na kuwauzia wenye pesa zao kwa ridhaa zao. Aidha, cha kushangaza ni kuwa 'lease' hiyo ilitolewa bila ya kulipwa fidia kwa mwananchi huyo ambaye ameshindwa kulitumia eneo hilo hadi hii leo. Aidha, huyo muwekezaji na yeye sio muwekezaji bali ni

dalali ambapo ameshindwa kufanya mradi wowote hapo isipokuwa anatafuta mteja ili kuweza kuliuza eneo hilo kwa fedha nyingi ambapo yeye binafsi hakulipa hata senti moja. Hapa ndiyo tunaona udhaifu wa sisi viongozi tunapopewa dhamana badala ya kuwasaidia wananchi wetu matokeo yake tunaangalia maslahi yetu kwa kushiri katika kuwapora mali zao wananchi wetu (wakwezi na wakulima).

Mheshimiwa Spika,

7. Pia, Kamati yangu imepata malalamiko ya mradi wa "Wave Resort" mradi ambao hata Mhe. Waziri umefika mbele yake na kuiahidi Kamati kuwa upo katika hatu ya utatuzi ila cha kusikitisha hadi anasoma bajeti yake haya yote tulioyataja ameshindwa kuyatatua. Nadhani kwa ruhusa yako masuala haya yapo mengi na Baraza hili kupitia Kanuni ya 111 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2016) uturuhusu iundwe Kamati Teule ili kwenda kuchunguza migogoro hiyo ambayo kwa asilimia zaidi ya 90 imesababishwa na Wizara wakiwemo Mawaziri pamoja na watendaji wao ili kuja na mapendekezo kwa Serikali juu ya nini cha kufanya ili kuweza kumaliza migogoro hiyo. Ingawa Kamati yangu inajua kuwa migogoro ya ardhi imeundiwa Mahkama yake, lakini hii migogoro ni tofauti kwani imesababishwa na Serikali ambapo Mawaziri ndio wanaotumia na kwa mujibu Kanuni ya 43(5) Serikali wakiwemo Mawaziri wanawajibika kwa Baraza la Wawakilishi na hili ndio jukumu letu.

Mheshimiwa Spika,

8. Kutokana na kuokoa muda naomba nimalizie jambo moja ambalo ni ukiukwaji mkubwa wa Sheria za nchi pamoja na za maadili ya uongozi wa Umma, Kamati yangu imegundua kuwa Waziri aliyepita aliwagaia maeneo mengi na makubwa watu wa karibu yake ambapo maeneo hayo yalikuwa yakimilikiwa na wananchi wengine na maeneo hayo Serikali haifaidiki na chochote, isipokuwa wamekaa bure na kuikosesha Serikali mapato makubwa ambayo yangeliweza kuongeza mapato ya Serikali kwakuwa maeneo hayo ni mengi nadhani yatachukua muda mrefu kuyataja tutayaambanisha kwenye hotuba yetu hii ili kuangalia Sheria za nchi zinasemaje ili maeneo hayo yalete tija kwa wananchi wote. Pamoja na hayo, pia Kamati yangu imegundua Serikali inakosa mapato mengi kwa watu ambao wamepewa "lease" kwa muda mrefu lakini wameshindwa kuyaendeleza maeneo na kuikosesha Serikali mapato ambayo ndio nguzo ya Uchumi wa nchi zote Duniani na pia miongoni mwao wako ambao hata hawalipii hizo "Lease" husika, hii ni hasara kubwa kwa Serikali yetu.

## PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa huduma zilizopangwa kutekelezwa kupitia programu hii ni huduma ya kusimamia matumizi bora ya nishati iliyo salama na rafiki kwa mazingira, kusimamia tafiti na kuendeleza matumizi ya nishati mbadala kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii, kusimamia na kuanzisha mpango wa utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, uimarishaji wa miundombinu ya maji mijini na vijijini, umarishaji na kuijengea uwezo ZAWA kujiendesha kibiashara, usambazaji wa umeme vijijini, uimarishaji na uendelezaji wa miundombinu ya umeme, kuanzisha na kusimamia miongozo ya kitaalamu kwa maendeleo ya mafuta na gesi asilia pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za mafuta na gesi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kama inavyofahamika hii ni miongoni mwa Programu muhimu kwa manufaa na maendeleo ya nchi yetu programu ambayo inaingiza mapato makubwa kwa Serikali ila bado utekelezaji wake unasuasua kwa kiasi kikubwa.

**MheshimiwaSpika,**

Kamati yangu inampongeza sana Dkt. Shein kwa kutuletea Sheria ya kuweza kusimamia masuala ya Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar na hivi sasa Serikali imeshaanza kuunda vyombo na Mamlaka ambazo zinatakiwa kuanza shughuli zake pamoja na kutengeneza Kanuni ambazo zitawavutia wawekezaji katika sekta hii mpya kwetu ya Mafuta na Gesi Asilia. Pia, Kamati yangu inaitaka Serikali kuweza kuzipatia pesa za kutosha taasisi hizo kwani kazi zao ni za kitaalamu zinahitaji vitendea kazi vya kisasa, wataalam waliokuwa wazuri, lakini pia wenye uzoefu katika masuala mbali mbali yanahusu mafuta na Gesi Asilia kwani kwa mafungu tuliyoyatenga kwa bajeti ya mwaka huu kwa kweli hatujawatendea haki kwani taasisi zinapokuwa mpya zinahitaji nyenzo za kutosha ili kuweza kujiandaa na utekelezaji wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika eneo hili la nishati ya mafuta na Gesi Asilia Serikali inatakiwa kuwekeza zaidi katika kuwasomesha vijana wetu wenye umri mdogo waliotoka vyuoni ili wawe na muda mrefu wa kuja kufanya kazi katika sekta hii na kupunguza kutegemea wataalamu kutoka nchi za nje ambao watakuja kuigharimu Serikali

pesa nyingi,sasa kwakuwa hivi sasa kuna vijana zaidi ya sitini tayari wameshamaliza masomo yao katika fani hii ya mafuta na Gesi Asilia basi tunaiomba Serikali kuwaajiri vijana wetu hawa ili kuanza kupata uzoefu lakini pia kuwatafutia mafunzo nje ya nchi ili wajekulitumikia Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, katika eneo hili tunamuomba Mhe. Waziri akija ajekutueleza kwa hivi sasa shughuli gani zimeshaanza katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia na vipi uitikiaji wa wawekezaji katika utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia lakini pia je kuna kampuni yoyote ambayo Serikali imeshampa kibali cha uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa visiwani kwetu?

**Mheshimiwa Spika,**

Lakini pia Waziri aje kutueleza kuhusu utafiti uliokuja kufanywa na ile ndege ya utafiti wa mafuta Serikali imeshakabidhiwa ripoti yoyote inaonyesha kama Mafuta na Gesi Asilia yapo hapa Zanzibar kwani wananchi wetu wanahamu kubwa ya kusikia kuwa Zanzibar yamegundulikana Mafuta na Gesi Asilia kuwa yapo ili waweze wananchi wetu kunufaika na rasilimali hiyo na kuondokana na umakini. Pia Mhe. Waziri aje kutuambia vipi kuhusu utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya Mafuta na Gesi Asilia na changamoto zake ili na wao washiriki kikamilifu katika kunufaika na rasilimali hizo lakini zaidi katika uhifadhi wa mazingira katika maeneo yao.

**Mheshimwa Spika,**

Kamati yangu kwa upande huu inaipongeza sana ZURA kwa utendaji wao wa kazi zaidi katika kusimamia ubora wa maji na mafuta kwani kwa kipindi kirefu tangu kuanzishwa kwa Taasisi hii ya ZURA hatujasikia kuadimika kwa mafuta wala kusikia kuwa mafuta machafu na vyombo vya moto kuharibika wakati huko nyuma ilikuwa ni jambo la kawaida kusikia maharibiko ya vyombo vya moto na kuadimika kwa mafuta. Lakini Kamati yangu pia inaishauri ZURA bado kuna tatizo la matumizi ya mashine ya kupimia mafuta kwenye Sheli zetu kwani inaonekana baadhi ya vituo vipimo vyao vinawadhulumu wananchi kwa hiyo tunaiomba Mamlaka hii kufanya kama wanavyofanya wenzao "EWURA" kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika vituo hasa vya mashamba kwani inaonekana kuna mchezo mchafu unafanyika, kuondoa kuwabinya wateja na watumiaji wa vyombo vya moto.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu pia inaipongeza tena ZURA kwa mpango wao wa kuliendeleza eneo la Mangapwani kwa nia ya kujenga Bandari itakayotumika kwa ajili ya kupakia na kupakulia mafuta kutoka kwenye Meli. Mradi ambao tunategemea utaweza kuleta tija na manufaa makubwa sana kwa Serikali yetu kwa hiyo tunawatia moyo ili msirudi nyuma. Hivyo, Mhe. Waziri akija atuambie "project" ile imefikia hatua gani.

Mheshimiwa Spika,
Pamoja na hayo, tunaipongeza ZURA kwa mara nyengine tena kwa kuja na wazo la kujenga jengo lao ambalo litaweza kusaidia sana kuondoa tatizo la ufinyu wa nafasi kwa taasisi mbali mbali zilizomo katika Wizara hii Ardhi, nalo suala hili pia Mhe. Waziri akija aje kutuambia wamefikia hatua gani.

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Mjini kutoka kwa wafadhili wetu kutoka India unatekelezwa kwa wakati na ndani ya muda uliowekwa ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wetu. Pamoja na hayo, Kamati yangu inaitaka Mamlaka hii katika bajeti hii kuweka utaratibu maalum wa kuvipa kipaumbele visima vyote ambavyo vilichimbwa kupitia mradi wa Ras Al khaimah viweze kufanya kazi iliyokusudiwa kwani visima hivyo vikiungwa umeme na kuekewa miundombinu ya mabomba basi tunaamini maeneo mengi ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba vitapata maji ya kutosha na kupunguza tatizo la maji kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika,
Lazima tuwe wawazi kwani tatizo la maji bado ni kubwa hasa katika Mji wetu wa Zanzibar hususan katika Mkoa wa Mjini Magharibi na tukizingatia bado makaazi ya watu yanaongezeka siku hadi siku katika Mkoa wetu huu. Hivyo basi, ni vyema kwa Mamlaka ya Maji kwa kushirikiana na Serikali za mitaa kuhakikisha vianzio vya maji vinalindwa kwani Kamati yangu ilipotembelea baadhi ya vianzio hivyo iligundua kuwa baadhi yake vimeshavamiwa na makaazi ya watu jambo ambalo linapelekea kina cha maji kupungua kila siku na kusababisha upungufu wa rasilimali hiyo muhimu kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia imegundua kuwa msitu wa Masingini pamoja na ule wa Mwanyanya kwa taarifa za wataalamu ndio msitu unaohifadhi kiasi kikubwa cha maji ardhini na ndicho kinachosaidia kupatikana kwa maji ila msitu huyo tayari nao umeshaanza kuvamiwa na ujenzi wa nyumba za makaazi jambo ambalo linaweza kusababisha uhaba wa maji. Hivyo, Kamati yangu inaitaka ZAWA kwa kushirikiana na Halmashauri husika kuzuia ujenzi wa aina yoyote karibu na msitu huo.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, Kamati yangu inaitaka ZAWA kuweza kununua "Pump" za maji zenye viwango bora ili kuepusha kuharibika mara kwa mara kwani wananchi wetu wanasumbuka sana kutokana na kuharibika au kuungua kwa "pump" hizo. Pamoja na hayo, Kamati inaitaka ZAWA kuharakisha mradi wa ubadilishaji mabomba ya kupitishia maji kwani mengi yaliopo yameshakuwa machakavu ikiwemo kuziba kwa calcium" ndani ya mabomba na hivyo kupelekea kupasuka na kuzuia kasi ya upitishaji wa maji kwenda kwa wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nikitoka upande huo naomba sasa niingia katika Shirika la Umeme Zanzibar ambalo ndio tegemeo kubwa la Serikali kwa ajili ya kutoa huduma za usambazaji wa umeme mjini na vijijini. Aidha, licha ya mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana, bado Shirika hilo linaendeshwa kihasara hali ambayo inaisababishia Serikali kukosa kufikia makusanyo yaliyojiwekea. Vile vile, Kamati inaendelea kuishauri Wizara kukaa pamoja na Shirika la Umeme na Idara ya Nishati kutafuta mbinu mbadala ya kuweza kuzalisha umeme wa jua, upepo pamoja na mawimbi ya bahari jambo ambalo litaisaidia Serikali kuwa na chanzo chengine cha umeme kuliko ilivyo hivi sasa ambapo tunategemea chanzo kimoja tu. Pia Shirika limekuwa likibambikiziwa gharama nyingine ambazo wala hazina msingi na kulibebesha Shirika madeni yasiyolipika.

**Mheshimiwa Spika,**

Hivyo, Kamati yangu pia inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza tena Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa busara zao na hekima zakuanza kulipa deni la Zanzibar kwenda TANESCO Tshs. 11.8 bilioni kati Tshs. 61.8 ya deni halisi. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hii iliyoanza kuchukuliwa ya kulipa deni hilo. Pamoja na pongezi hizo kwa Serikali, Kamati

yangu inaitaka Wizara ya Fedha ili kuiokoa ZECO na kubeba mzigo mkubwa wa madeni basi ni vyema kwa upande wa taasisi za Serikali, Wizara ya Fedha ikaweza kulipa moja kwa moja ZECO kwa zile taasisi ambazo hazijaungiwa mita za tukuza ili kulipa nguvu Shirika kuweza kutoa huduma bora kwa wakati na pia kuweza kulipa madeni ya TANESCO.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia  inaipongeza ZECO kwa kuweka mkakati wa kulipa 'current Bill' na pia malipo ya ziada kwa TANESCO ili kuweza kulimaliza deni hilo kwa muda waliojipangia. Kwa hiyo na sisi wananchi tuisaidie ZECO kwa kulipa bili zetu kwa wakati ili kuliwezesha Shirika kulipa madeni yake kwa wakati. Pia bila ya kusahau, Kamati yangu inapenda kumpongeza Mhe. Professor Muhongo, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini kwa jinsi akivyoweza kulisimamia suala la deni halisi la umeme la ZECO kwa TANESCO. Pamoja na mtihani ya uwajibikaji kazini iliyomkuta, lakini sisi kama Kamati tunathamini mchango wake kwa Zanzibar. Tunamuomba Mungu ampe subira kwani huo ndio uwajibikaji wetu kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pamoja na pongezi kwa ZECO lakini pia inautaka uongozi wa Shirika na Bodi kuangalia kwa karibu utendaji wa Shirika hasa katika kufuatilia masuala ya "Tender" na manunuzi ya Shirika kwani inaonekana matumizi yanazidi kuwa makubwa ambapo kwa upande mwengine kuna mkakati wa kulipa Deni la TANESCO. Pamoja na hayo, pongezi zetu kwa ZECO kwa kufanikisha usambazaji wa umeme vijijini kwa asilimia 80 na tunategemea ifikapo 2020 kuweza kufikia zaidi ya asilimia 90.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

**Mheshimiwa Spika,**

Dhumuni kuu la Programu hii ni kuhakikisha usimamizi ulio bora na imara juu ya mambo yote yanayohusiana na mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuweka usimamizi endelevu wa masuala hayo. Ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2106/2017, programu hii imetengewa Tshs. 1,598,298,000 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,**

Licha ya fedha hizo kutengwa kwa Mamlaka hiyo pamoja na Idara yake, bado changamoto zinaendelea kuwepo na wala hazipungui. Miongoni mwa Changamoto hizo ni wakurungezi wawili kukaa katika ofisi moja hali ambayo inawakosesha faragha ya utendaji kwa wakuu hao jambo ambalo Kamati yangu hailipendelei hata kidogo kwani limekuwa ni suala la muda mrefu lakini Wizara inashindwa kulichukulia hatua kwa kulitafutia ufumbuzi. Changamoto nyingine ni uchimbaji wa mchanga kiholela kwa baadhi ya maeneo mbali mbali hasa Kinuni na kusababisha mashimo ambayo ni hatari kwa wakaazi wa maeneo hayo wakati wa mvua, pia utupaji wataka ovyo katika maeneo ya mjini na vijijini pamoja na ukosefu wa elimu ya mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na Changamoto hizo Kamati yangu inamuomba Mhe. Waziri kuweza kuwatafutia jengo jengine itakalokuwa na nafasi kubwa ya kuhimili idadi kubwa ya watendaji. Aidha, Kamati haitosita kuishauri Mamlaka kwa kushirikiana na Idara kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi, kwani miongoni mwa changamoto kubwa Duniani kwa hivi sasa ni mabadiliko ya tabianchi ambapo katika Mkutano uliofanywa nchini "Mexico" mwezi uliopita ni kuwa jamii ipatiwe elimu ya mazingira ili kupunguza maafa pale yanapotokea.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia Kamati yangu imefanya utafiti mdogo katika maeneo mengi ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kwenye maeneo ya fukwe za bahari zinaendelea kula nchi miaka kila ikienda na haya yote kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na ujenzi usiofuta Sheria na taratibu za mazingira ambapo mradi wowote unatakiwa kujengwa nje ya mita 30 kwa maeneo ya fukwe na mita 10 kwa maeneo ya mwambao. Lakini katika eneo hili wawekezaji wengi wameshindwa kufuata Sheria ya ujenzi katika maeneo ya fukwe ambapo wamekuwa wakijenga nje ya utaratibu. Matokeo yake maji ya bahari yamekuwa yakipanda juu kila siku zikienda na kuvamia mashamba ya watu na kuwakosesha wananchi kulima mashamba yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kadhia nyengine ya uharibifu wa mazingira ni kuwa kumeanza kujitokeza tatizo kwa wananchi wa Jimbo la Mtoni hivi sasa zaidi ya nyumba 80 zimekuwa

zikiingia maji bahari kutokana na mradi mkubwa unaoendelea hapo katika eneo la "Mtoni Marine". Mradi ambao umesababisha nyumba hizo hivi sasa kuvamiwa na maji ya bahari.

**Mheshimiwa Spika,**

Jambo hili ni kubwa na limeleta taharuki kubwa kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yaliokaribu na mradi huo. Kwa hiyo, Kamati yangu inamtaka Waziri wa Ardhi, Waziri wa Utalii, Waziri wa Mawasiliano pamoja na Waziri wa Fedha kuliundia Tume maalum na kuleta Barazani kuona ni kiwango gani cha athari ya mazingira na hatua gani za haraka zinachukuliwa juu ya kulinda makaazi ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuanza kufanya uteuzi wa baadhi ya wasimamizi wa Mamlaka za kusimamia masuala ya Mafuta na Gesi hapa Zanzibar, lakini kasi ya ukamilisha wa vyombo hivyo ni ndogo kwani bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwa jamii na Taifa kwa jumla. Lakini pia inaonekana bado Serikali haijalipa umuhimu mkubwa suala hilo kwani mafungu ya fedha waliyotengewa ni madogo hasa ukizingatia taasisi hizo ni mpya kwa hiyo zinahitaji miundombinu ya kisasa ili kuweza kufanya shughuli zake kwa ufanisi mkubwa, kuanzia wataalamu, vifaa vya kisasa pamoja na usafiri wa uhakika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuja na mipango mipya ya kuipanga miji yetu ili iwe ya kisasa na yenye huduma bora, ingawa kumekua na baadhi ya changamoto hasa katika kuhamisha makaazi ya watu ikiwemo wafanya biashara inaonekana ushirikishwaji unakuwa mdogo na kuleta malalamiko makubwa kwa wananchi wetu pamoja ya kuwa hawapingani kile kinachotaka kufanywa na Serikali. Lakini pia Kamati yangu inaitaka Serikali kuwa kitu kimoja hasa katika matumizi na mipango ya kuendeleza maeneo yanayogusa hifadhi ya Mji Mkongwe kwani kuna baadhi ya Wizara hufanya maamuzi ya matumizi ya Mji Mkongwe bila ya kuwashirikisha Mamlaka, jambo ambalo linachelewesha miradi hiyo na wakati mwengine kupelekea kuwavunja moyo wawekezaji na pia kuwatia hasara kwa kucheleweshwa kufanya miradi yao mfano Hoteli ya Bwawani, Jumba la Treni Darajani na mradi wa ujenzi Darajani Corridor.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia inaishauri Serikali katika kupanga matumizi bora ya ardhi basi ni vyema Serikali kushirikiana na Shirika la Nyumba la Zanzibar kuharakisha mpango wao wa kutafuta wafanyabiashara au fedha na kuanza kujenga majengo ya kisasa katika maeneo yetu ya nga'mbo na kuwauzia au kuwakodisha wananchi ili tuweze kuwa na makaazi bora yanayoendana na karne hii ya sayansi na technologia, ambapo yapo mashirika na taasisi za kifedha ambayo yapo tayari kushirikiana kuifanya kazi hiyo. Kwa hivyo ni vyema kuwepo mashauri ya pamoja na ya karibu baina ya Idara ya Mipango Miji na Shirika la Nyumba la Zanzibar ili kufanikisha mpango huo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa Bajeti basi wale Wazee wa Mahakama ya Ardhi waweze kuwalipa mafao yao yote ili kuwapunguzia makali ya maisha hasa ukizingatia kuwa wanalitumikia Taifa letu kwa muda mrefu lakini pia kazi wanayoifanyia ni kubwa. Pamoja na hayo, tunaipongeza Wizara hii kupitia Katibu Mkuu baada ya kuona wazee wetu hawa wanasumbuka katika kuwalipwa mafao yao kwa kuwaekea fungu maalum kwa mwaka huu wa bajeti ya 2017/2018 ambapo mwanzo hazikuwemo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ya Ardhi na Mawasiliano imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018, na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wako wote waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimaye kuipitisha Bajeti hii. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza viongozi na watendaji wa Wizara hii tena kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo naomba kuunga mkono pamoja na kuwatakia Waheshimiwa wote pamoja na wananchi Ramadhani njema na afya tele.

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………..,
Mhe. Hamza Hassan Juma,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ardhi na Mawasiliano,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**